

## **WIZARA YA ELIMU**

### **WILAYA YA MUHANGA**

### **MTIHANI WA KISWAHILI**

### **KIDATO CHA KWANZA**

**Maelezo : Mthani huu unaundwa na sehemu kuu mbili**

#### **I . Ufahamu wa mwandiko namsamiati/30 alama**

#### **II. Sarufi na maelezo ya lugha /30 alama**

##### **I Mwandiko.**

Mimi ninaitwa Kwizera. Mimi ninasoma katika kidato cha kwanza. Shule yetu inaitwa shule ya Sekondari ya Gikondo. Kayitare ni kiranja wa darasa letu. Yeye hutuwakilisha katika mikutano mingi ya shule. Katika mikutano na mkuu wa shule, yeye huliza maswali mazuri kwa sababu yeye ni mwanafunzi hodari sana. Mimi ninaelewa vizuri masomo yote; Kiswahili, Kinyarwanda, Kiingereza, Hisabati, Jiografia, Historia na mengine.

Shule yetu ina viongozi wazuri. Baadhi ya viongozi wa shule yetu ni mkuu wa shule, naibu wa mkuu wa shule, mwalimu wa mitaala ambaye ni mwalimu wa taaluma, mwalimu wa nidhamu, mhasibu na mkutubi anayesimamia maktaba ambapo vitabu vyetu huhifadhiwa. Shule yetu ina vitabu vingi.

Kila asubuhi, mkuu wa shule hutukagua ikiwa tumevaa sare. Yeye pia hutushauri kupenda masomo yetu, kusaidiana na kufanya kazi kwa bidii. Mwalimu wa mitaala hupanga masomo ya kila muhula. Mwishoni mwa kila muhula sisi hufanya mitihani. Mhasibu wa shule hupokea karo za wanafunzi. Mwalimu wa nidhamu huwaadhibu wanafunzi wanaofanya makosa; wanafunzi watukutu, wanafunzi wanaotoroka shuleni na wale wanaopiga kelele darasani.

Mwalimu mshauri wa wasichana, huchunguza nidhamu ya wasichana. Yeye hutatua shida zao shuleni, hutushauri kuwa na mienendo mizuri, huchunguza wakati wa kuingia mabwenini na kadhalika. Mwalimu mshauri wa wavulana huchunguza nidhamu ya wavulana na kupanga michezo shuleni kwa kushirikiana na mwalimu mshauri wa wasichana. Wakati wa chakula cha mchana na chakula cha jioni, walimu wa zamu huingia bwaloni kuchunguza chakula chetu na kutushauri kuheshimiana wakati wa kula. Mimi ninapenda sana viongozi wetu shuleni.

#### **A) Zoezi la ufahamu /20 alama**

- 1.Kwizera anasomea wapi?
- 2.Yeye anasoma katika kidato gani?
- 3.Kiranja wao ni nani?
- 4.Kwizera anaelewa vizuri masomo gani?
- 5.Viongozi wao ni nani?
- 6.Mwishoni mwa kila muhula wanafunzi hufanya nini?
- 7.Katika mikutano na mkurugenzi, kiranja wao hufanya nini?
- 8.Mkuu wa shule anaitwa nani?

9. Mkuu wa nidhamu huwaadhibu wanafunzi gani?

10. Walimu washauri huingia bwaloni kufanya nini?

B) Msamaiti: 10 alama

1) Tumia maneno yafuatayo katika sentensi yako sahihi

a) Mukua wa shule

b) kiranja

c) Karo

C) Daktari

E) Anawachunguza

II) Sarufi na maelezo ya lugha /30 alama

1) Waamkie wenzako kwa salamu zifuatazo kisha fanyeni igiza la kuamkiana /3 alama

a) Habari za jioni?

b) shikamoo

c) sabalheri !

2) Weka sentensi hizi katika umoja au wingi /6 alama

a) Kwa heri maria

b) Habari yako

c) Mhali gani ?

d) Hamjambo walimu ?

3) Tafiti na uandike ya sauti ambatano zifuatazo /3 alama

a) [ nj ] b) [ sw ] c) [ mw ]

4) Tafuta majibu ya maamkizi yafuatayo /5 alama

a) waambaje? b) Hodi c) pole! d) salama? c) Kwa heri !

5) jaza nafasi zilizoachwa wazi na nafsi sahihi / 3 alama

a) Ninaitwa famia ( Mimi) : Tunaitwa samia (.....)

b) Unaitwa mufisha( wewe) : Mnaitwa Mufisha (.....)

- c) Anaitwa gatete ( yeye) wanaitwa gatete ( .....)
- 6) Chagua jibu sahihi kati yay ale yaliopendekezwa mabanoni / 2alama
- a) Musafiri amefanya .....( Zoezi/ dabtari) lakiswahili.
- b) Wanafunzi ..... ( wajambo / hawajambo)
- c) kilamwanafunzi anachagua .....) jibu/ kiti sahihi
- d) Daftari la mutoni ..... ( linanyesha/ limeharibika).
- 7) Eleza vivunishi vya sifa tatu kisha. Uvitumie katika sentensi yako sahihi /3 alama
- 8) Andika majina matano ya siku za wiki /5 alama

**Bahati njema Heli na fanaka zasikukuu ya pasaka !**